Nipashe Julai 3, 2025



Pg 3

# LATRA yatangaza kampuni 3 kutumia tiketi mtandao

Na Imani Nathaniel

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetangaza kampuni tatu za mifumo ya tiketi mtandao zimekamilisha masharti yote kisheria na kupatiwa vibali rasmi vya kutoa huduma hizo kwa mujibu wa Kanuni za Tiketi Mtandao za mwaka 2024.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano wa LATRA, Salum Pazzy, alisema kampuni hizo ni Ottap Agency Company Limited, Hashtech Tanzania Limited, na Iyishe Company Limited. Kampuni hizo zimeruhusiwa kufanya malipo ya vibali na baada ya kukamilisha malipo hayo, watakabidhiwa vibali rasmi vya kutoa huduma ya tiketi mtandao nchini.

Taarifa hiyo imeeleza kuwa hatua hiyo ni utekelezaji wa Kanuni za Tiketi Mtandao zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 20 la Desemba 1, 2024. Kanuni ya 5 inazitaka kampuni zinazotoa huduma za tiketi mtandao kuwa na kibali kutoka LATRA. Miongoni mwa vigezo ni mifumo kuwa na ulinzi dhidi ya uvamizi wa kimtandao pamoja na uwezo wa kuunganishwa na mifumo ya serikali.

Kwa mujibu wa LATRA, kampuni nyingine sita zimeonesha mwelekeo mzuri wa kukidhi vigezo hivyo, ingawa zina changamoto ndogo. Kampuni hizo ni AB Courier Express Limited, Busbora Company Limited, Logix Company Limited, Mkombozi Infotech Company, Sepatech Company Limited na Web Corporation Limited. Kampuni hizi zimepewa muda wa siku 14 kuanzia Julai 2, 2025 kukamilisha matakwa yote ya kisheria, la sivyo zitasitishiwa huduma hiyo.

Aidha, kampuni mbili, Duarani Innovative Company na Itule Company, zimebainika kuwa na changamoto kubwa zinazowafanya kukosa sifa za msingi. LATRA imezipa muda wa siku saba kama kipindi cha matazamio, na iwapo hazitakamilisha matakwa hayo, zitasitishwa kutoa huduma na wateja wao kushauriwa kuhamia kwa watoa huduma waliokamilisha utaratibu.

"Tunahimiza wasafirishaji wote na watoa huduma kutumia mifumo ya tiketi mtandao iliyotambuliwa kisheria ili kuepuka usumbufu wakati wa ukaguzi. Kampuni zisizotajwa hazitambuliki kisheria," alisema Pazzy.

LATRA imeeleza kuwa watoa huduma wote wanapaswa kuunganisha mifumo yao na mfumo wa tiketi mtandao wa LATRA (CeTS), sambamba na kuingiza taarifa zote za mabasi katika mfumo jumuishi wa LATRA (UTS). Mfumo huu umesanifiwa kurahisisha upatikanaji wa tiketi kwa watumiaji wa huduma za usafiri wa treni za SGR, MGR na mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani. Wananchi wanaweza kufikia mfumo huo kupitia tovuti ya tiketi.latra.go.tz kwa kutumia simu janja au kompyuta.

LATRA pia imeeleza kuwa itaendelea kushirikiana na wamiliki wa mifumo na wataalamu wa Serikali kuhakikisha huduma bora na salama kwa wasafirishaji, abiria na Serikali. Ukaguzi na ufuatiliaji utaendelea kufanyika ili kudhibiti utekelezaji wa kanuni na kuchukua hatua za kisheria kwa wanaokiuka masharti.